END TB

# HALI YA KIFUA KIKUU NCHINI NA, RASILIMALI




eannaso


NTLP
NATIONAL TUBERCULOSIS & LEPROSY PROGRAMME

Tanzania TB Community Network

Stop TB Partnership hosted by UNOPS

## KIFUA KIKUU NI NINI

Kifua kikuu (TB) ni ugonjwa wa kuambukiza unaosababishwa na vimelea aina ya bakteria waitwao “Mycobacterium tuberculosis”. TB ni ugonjwa wa kuambukiza unaosambaa kutoka kwa mtu mmoja mwenye vimelea kwenda kwa mtu mwingine kwa njia ya hewa anapokohoa, kucheka, kuongea, kupiga chafya, kuimba na matendo yanayofanana na hayo. Hata hivyo, kikohozi huchukua nafasi kubwa katika maambukizo ya TB. Mgonjwa wa TB ambaye hajaanza matibabu ni chanzo kikuu cha maambukizo ya TB.





## HALI YA TB NCHINI


TB ni tatizo kubwa la afya ya jamii duniani kote ambapo mwaka 2018 watu milioni 9 waliugua TB. Tanzania ni mojawapo kati ya nchi 30 zenye wagonjwa wengi kulingana na takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO). Makadirio ya WHO ni kwamba, mtu mmoja mwenye kifua kikuu ambaye hayupo kwenye matibabu, anaweza kuwaambukiza watu kati ya 10-20 kwa mwaka.

Hapa nchini Tanzania kwa mjibu wa takwimu za Mpango wa Taifa wa kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa wastani wa watu 142,000 huugua kifua kikuu kila mwaka, sawa na wastani wa wagonjwa 389 kila siku. Asilimia 47 sawa 67,000 ya watu wenye kifua kikuu wanaachwa bila kupimwa na kutibiwa kila mwaka ukiachilia mbali juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali na washirika kuudhibiti ugonjwa huu.

## KIWANGO CHA MATIBABU YA TB NA MAFANIKIO


Lengo la Shirika la Afya Duniani lilikuwa ni kuhakikisha kuwa asilimia 90 ya wagonjwa wote wa TB wanafikiwa na kupatiwa matibabu kufikia mwaka 2025. Hapa Tanzania kwa mjibu wa takwimu za WHO za mwaka 2018, ni 57% tu ya watu wanaokadiriwa kuwa na TB wamepata matibabu ya Kifua Kikuu. Aidha katika watu waliogundulika kuwa na TB na kupatitwa matibabu, 90% kati yao wametibiwa na kupona kabisa.




## KIFUA KIKUU SUGU

Hii ni TB isiyotibika kwa dawa za kawaida za TB kutokana na usugu wa vimelea kwa dawa hizo. Kifua kikuu (TB) sugu kinaongezeka kwa kasi kubwa na hivyo kuleta changamoto katika matibabu na udhibiti wa TB. Kwa mjibu wa takwimu za WHO, inakadiriwa kuwa Jumla ya watu 1,900 walipata Kifua Kikuu sugu (kifua kikuu kisichosikia dawa) mwaka 2018. Hata hivyo, ni wagonjwa 449 pekee wenye TB sugu waligunduliwa na 409 kati yao waliingizwa kwenye matibabu. Hii inaashiria kwamba pia kuna watu wenye TB Sugu bado hawajagunduliwa na kupatiwa matibabu. Changamoto kubwa ni uwezo mdogo wa kuwatambua na kuwatibu wagonjwa wenye TB sugu katika ngazi zote za huduma ya afya. Kimsingi TB sugu ni tatizo linalosababishwa na binadamu. Sababu kuu ni umezaji duni wa dawa na kuambukizwa vimelea ambavyo tayari vina usugu.





## MAAMBUKIZI MSETO YA TB NA VVU

Maambukizo ya VVU yamesababisha ongezeko la wagonjwa wa TB duniani hasa katika ukanda wa kusini mwa jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania. Inakadiriwa kuwa asilimia 50 ya wagonjwa wa TB wana maambukizo ya VVU duniani kote. Takwimu za WHO za mwaka 2018 zinaonyesha kuwa wagonjwa 40,000 wa TB walikuwa na maambukizo ya VVU. Hata hivyo ni watu 20,695 kati yao waligundulika na 20,337 waliwekwa kwenye matibabu.

## VIFO VITOKANAVYO NA KIFUA KIKUU

Zaidi ya hayo, kifua kikuu husababisha vifo 70 kwa siku kitaifa ambapo ni sawa na watu watatu wanakufa kila saa nchini. Mwaka 2018, takwimu zinaonyesha TB ilisababisha vifo 38,000 na vifo 16,000 kati hivyo vilikuwa ni vya watu wenye VVU.




## UFADHILI WA KIFUA KIKUU (MAMILIONI YA DOLA ZA KIMAREKI), 2011-2019

| MWAKA | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | GLOBAL FUND | MAHITAJI | UPUNGUFU |
|---|---|---|---|---|---|
| 2011 | 7.3 | 11.799 | 3.801 | 34 | 11.4 |
| 2012 | 8.1 | 7.494 | 4.506 | 42 | 21.9 |
| 2013 | 8.3 | 1.504 | 5.896 | 57 | 41.3 |
| 2014 | 8.2 | 0 | 0.556 | 58 | 49.244 |
| 2015 | 8.5 | 0 | 9.541 | 61 | 42.959 |
| 2016 | 2 | 3.992 | 12.008 | 40 | 22 |
| 2017 | 0.38 | 0 | 11.493 | 70 | 58.127 |
| 2018 | 1.488 | 0 | 25.083 | 63.941 | 37.37 |

*Chanzo: WHO, Global Fund*

Mwaka 2018 kiasi dola za Kimarekani milioni 63.941 zilihitajika kwa ajili ya kukabiliana kikamilifu na janga la TB nchini Tanzania. Hata hivyo ni 41.6% ya fedha zinazohitajika zilipatika zikichangiwa na 3% fedha za ndani na 39% fedha za nje kutoka kwa wahisani na kuacha pengo la fedha kwa 58.4%.

## DONDOO MUHIMU KUHUSU TB

### DALILI ZA KIKUA KIKUU

- Kukohoa kwa wiki 2 au zaidi
- Homa za mara kwa mara kwa wiki 2 au zaidi
- Kutokwa na jasho jingi kuliko kawaida hasa usiku
- Kupungua/kutoongezeka uzito au kudumaa
- Kukohowa makohozi yaliyochanganyika na damu
- Kutokwa jasho jingi kuliko kawaida hasa nyakati za usiku.
- Kwa watoto Kukosa raha, kulia lia kutochangamka na kukosa raha.

### TIBA YA KIKUA KIKUU

- Matibabu ya kifua kikuu ni miezi sita
- Mgonjwa anatakiwa kunywa dawa kila siku bila kukosa
- Ni muhimu kumaliza dozi au matibabu kama ilivyoelekezwa na mhudumu wa afya
- Kumbuka, kuacha kunywa dawa za kifua kikuu kikamilifu kunaweza kusababisha vimelea kuwa sugu na hivyo kuambukiza watu wengine
- Tiba ya kifua kikuu inapatikana bila malipo yoyote katika vituo vya huduma za afya vya serikali na binafsi
- Matibabu yanatolewa kila siku chini ya usimamizi
- Mgonjwa anaweza kusimamiwa na mtu aliyemchagua mwenyewe nyumbani.

### JINSI YA KUZUIA MAAMBUKIZI YA KIFUA KIKUU

- Funika mdomo na pua kwa kitambaa unapokohoa au kupiga chafya
- Kama unakohoa kwa wiki 2 au zaidi, wahi kituo cha huduma za afya.
- Kugundua wagonjwa wote wenye dalili za kifua kikuu mapema na kuwatibu kikamilifu
- Kuepuka misongamano isiyokuwa ya lazima
- Epuka kutema mate au makohozi ovyo
- Kuishi kwenye mazingira safi na kuhakikisha nyumba zetu zinakuwa na mzunguko wa hewa pamoja na mwanga wa kutosha.
- Kuchanjwa dawa ya kinga ya kifua kikuu (B.C.G.) kwa kila mtoto mchanga. Hakikisha hata kama mtoto anazaliwa nyumbani apelekwe kituo cha tiba kwaajili ya chanjo
- Kula chakula bora
- Tumia dawa za TB kama ulivyoelekezwa na mtoa huduma za afya, TB inatibika na kupona kabisa.
- Unapoona dalili zinazofanana na za kifua kikuu wahi hospitali mapema kwa ajili ya vipimo na matibabu;

# MAKUNDI YALIYO KATIKA HATARI ZAIDI

TB inaathiri zaidi watu wa hali ya chini, wanaoishi kwenye mazingira duni, na wanaougua magonjwa mengine. Watu ambao wana vimelea vya TB wako kwenye hatari ya kuugua TB kwa 10% katika kipindi cha maisha yao. Hata hivyo watu wenye upungufu wa kinga mwilini kama vile WAVIU, wenye utapiamlo,wagonjwa wa kisukari au watu wanaovuta sigara wako kwenye hatari kubwa zaidi ya kuugua. Zaidi ya watu bilioni 2 duniani (30%) wana maambukizi ya TB, Hapa nchini, inakadiriwa kuwa zaidi ya watu milioni 18 wana maambukizi
ya TB.




# DHANA POTOFU KUHUSU TB

## BAADHI YA DHANA POTOFU KUHUSU TB KATIKA JAMII YETU YA TANZANIA ZINAHITAJI KUREKEBISHWA NI PAMOJA NA:

| DHANA POTOFU | UKWELI |
|---|---|
| Kila mgonjwa wa TB ana VVU | Si wagonjwa wote wa TB wana maambukizi ya VVU |
| TB ni ugonjwa wa laana au wa kulogwa | TB si ugonjwa wa laana wala wa kulogwa, bali ni ugonjwa wa kuambukiza kwa njia ya hewa unaosababishwa na vimelea vya bacteria aitwaye Mycobacterioum tuberclosis. |
| Kuchangia vyombo vya chakula ueneza ugonjwa wa TB | Kuchangia vyombo vya chakula hakuenezi ungonjwa wa TB, bali huenezwa kwa njia ya hewa |
| Epuka kujamiana wakati wa matibabu ya TB | Matibabu ya TB hayamzuii mgonjwa wa TB kujamiana |
| Mgonjwa wa TB hatakiwa kufanya kazi wakati wa matibabu ya TB | Matibabu ya TB hayamzuii mgonjwa wa TB Kufanya kazi |
| Kifua Kikuu ni ugonjwa wa maskini. | ugonjwa huu unaathiri kila mtu, na unapatika kila sehemu duniani. Ni suala la kila mmoja wetu! |
| | Matibabu ya ugonjwa wa Kifua Kikuu inapatikana bure nchini Tanzania. |

## MAREJEO

WHO Global TB Report 2019
Stop TB Partnership - http://www.stoptb.org/resources/cd/
Shirika la Afya Duniani (www.who.int/tb)
Stop TB Partnership (www.stoptb.org)
Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma (www.ntlp.co.tz)

# NOTES

## WASILIANA NA NASI

Tanzania TB Community Network (TTCN)

Hosted by EANNASO

Plot # 1 Olorien, Kijenge | Off Njiro Road

P.O Box 6187 | Arusha, Tanzania

+255 739 210598 ttcn.tanzania@gmail.com ttcntanzania


END TB

Tanzania TB Community Network